Jinsi ya kufungua akaunti ya benki

Juni 2010

Opening a bank account - Swahili

Kama una hadhi ya ukimbizi, ulinzi wa wahisani, kuondoka kwa hiari (DLR) au una kibali cha kuishi kabisa (ILR), una haki ya kufungua akaunti ya benki nchini Uskoti au sehemu yoyote ya Uingereza.

Hata hivyo, kabla ya kukufungulia akaunti ya benki, wanahitaji kuhakikisha kitambulisho chako na anwani yako.

Ukurasa huu unaonyesha ni hati gani utahitaji ili kufungua akaunti ya benki, jinsi ya kufungua akaunti na jinsi tunavyoweza kukusaidia.

Ninahitaji nini ili kufungua akaunti ya benki?

Kila benki ina orodha yake ya hati zinazohitajika kama kitambulisho na benki nyingine zinaweza kuhitaji maelezo zaidi kuliko wengine. Kwa kawaida unapaswa kupatia benki hati zinazothibitisha :

- kitambulisho chako;
- Hali yako ya uhamiaji; na
- anwani.

Fahamu kuwa benki kwa kawaida zitakubali hati zako asili pekee au nakala zilizotiwa saini.

Utahitaji kuonyesha **angalau thibitisho moja la kitambulisho** kama vile:

- Barua ya Ofisi ya Nyumbani ya kuthibitisha hali yako (hali ya ukimbizi, ulinzi wa uhisani, uondokaji wa hiari au uondokaji usio na mwisho wa kukaa) na idhinisho la kufanya kazi – hati asili au nakala iliyotiwa saini na Ofisi ya Nyumbani;
- Hati ya Utambulisho ya Ofisi ya Nyumbani – hati asili au nala iliyotiwa saini na Ofisi ya Nyumbani iliyo na nambari ya rejeleo, tarehe yako ya kuzaliwa na tarehe ya mwsho ya hati hiyo;
- Barua ya taarifa ya faida inayothibitisha haki yako ya faida; au
- Hati ya Hali ya Uhamiaji.

Scottish Refugee Council is a charity registered in Scotland.
Registered Charity: SC008639

Pia utahitaji kuonyesha **angalau thibitisho moja la anwani** kama vile:

- Barua kutoka kwa Ofisi ya Nyumbani ikionyesha jina lako na anwani yako ya sasa;
- Hati za madai zinazoonyesha jina lako na anwani ya sasa;
- Barua kutoka kwa wakala wa serikali, kwa mfano kutoka kwa Kituo cha Kazi, ikionyesha jina lako na anwani yako ya sasa; au
- Mkataba wa upangaji unaoonyesha jina lako na anwani yako ya sasa.

Benki inaweza kuitisha maelezo zaidi ya haya, kwa mfano, thibitisho la mapato yako.

Nitaenda wapi ili kufungua akaunti ya benki?

Utahitaji kuzuru tawi la benki ambayo umechagua na upeleke nyaraka zinazoonyesha wewe ni nani na mahali unapoishi kama ilivyoelezwa hapo juu. Lloyds TSB na Barclays ni mifano ya benki ambazo unaweza kuzingatia. Unaweza pia kwenda ili kujadiliana kuhusu kufungua akaunti au unaweza kupiga simu ili kupanga miadi kabla.

Tondoti za Mawasiliano za tawi lako la mtaa zinaweza kupatikana katika kitabu cha orodha za simu au katika tovuti ya benki hiyo.

Inachukua muda gani kufungua akaunti?

Hali ya uandikishaji hulingana na benki unayokwenda lakini kama una nyaraka zinazofaa; haiwezi kuwa kwa kawaida zaidi ya wiki 2-3.

Iwapo ombi lako linahitaji kurejeshwa kwa idara maalum kwa mazingatio zaidi, inaweza kuchukua muda zaidi ili kufungua akaunti hiyo. Wafanyakazi wa benki watakujulisha iwapo watapendekeza ombi lako na watakueleza sababu ya kufanya hivyo. Wanapaswa pia kujua itachukua muda gani kwao kufanya uamuzi kuhusu ombi lako.

Nimepewa akaunti msingi ya benki, ninaweza kuifanyia nini?

Akaunti msingi ya benki hutoa huduma za msingi za benki. Unaweza kuitumia kulipia na kutoa pesa.

Ukiwa na akaunti msingi ya benki unaweza:

- Kupata pesa kulipwa moja kwa moja kwenye akaunti yako kutoka kwa mahali pa nje kama vile wakala wa faida au muajiri;
- Kulipa pesa kwa njia ya elektroniki kwa watu wengine kupitia ‘maagizo ya benki’ au ‘uhamishaji’;
- Kuruhusu watu wengine kutoa pesa moja kwa moja kutoka kwa akaunt yako kupitia ‘udaiaji wa moja kwa moja’; na
- Kupokea kadi ya mdaiwa ili kukuruhusu kutoa pesa kutoka kwa mashini za pesa. Unawez a pia kununua vitu kwenye mtandao au kwenye maduka (uliza kwenye benki).

Nitalipia huduma nitakazotumia?

Akunti nyingi za msingi ni bure. Huhitaji kulipa ili kutumia mashini nyingi za pesa katika Uingereza. Hata hivyo, benki yako inaweza kukulipiza kiasi kidogo cha pesa iwapo huna pesa za kutosha kwenye akaunti yako wakati malipo ya moja kwa moja ya kadi ya mdaiwa ambayo umeithinisha yamekataliwa kwa sababu ya ukosefu wa pesa kwenye akaunti yako.

Chaguo zangu ni zipi iwapo siwezi kufungua akaunti ya benki?

Iwapo huwezi kufungua akaunti ya benki, unaweza kutoa ombi la kufungua akaunti ya kadi ya posta. Hii ni aina rahisi sana ya akaunti kwa wale wanaopokea faida, pensheni za serikali, malipo ya ushuru, ambao hawawezi kufungua akaunti ya benki. Hakuna malipo mengine, kama vile faida ya makazi, pensheni za kazi, au mshahara kutoka kwa muajiri wako yanaweza kulipiwa huku. Pia huwezi kuweka pesa kwenye akaunti hii.

Iwapo unapokea faida, uliza Kituo cha Kazi cha mtaa wako kukupa ‘barua ya mualiko’, ambao utakuruhusu kufungua akaunti ya kadi ya posta. Peleka mualiko huu pamoja na nyaraka ya hali yako ya uhamiaji kwa ofisi ya posta ya mtaa wako ili kufungua akaunti hiyo.

Akaunti ya kadi ya posta itakuruhusu kutoa pesa, bila mapilo, katika ofisi yoyote ya posta kwa kutumia kadi ya mdaiwa watakayokupa.

Je ninapohama?

Punde unapofungua akaunti yako ya benki, *kila mara* julisha benki yako kwa barua unapobadilisha anwani, haraka iwezekanavyo.

Halmashauri ya Wakimbizi ya Uskoti inaweza kunisaidia vip?

Iwapo tayari umetuma ombi la akaunti ya benki na hujafanikiwa kufungua moja, unaweza kuwasiliana nasi kwa ushauri. Unaweza kuwasiliana nasi katika **simu yetu ya bure: 0800 085 6087**; nambari hii ni bure tu kwa kutoka kwa simu ya ardhi.

Tunaweza kukupangia miadi na benki ili kujadili chaguo na kuambatana nawe kwa miadi yako ili kukusaidia. Fahamu kuwa sisi hutoa usaidizi huu **baada** yako kujaribu kufungua akaunti na hujafanikiwa.

Hudhuria warsha ya bure ya fedha

Iwapo ungependa kujua zaidi kuhusu akaunti za benki, usiamizi na ukopaji wa pesa au hata kuchukua hatua za kwanza za kuanza biashara, warsha zetu Mipango ya Mafunzo ya Pesa ni chanzo kizuri.

Kwa maelezo zaidi tuma barua pepe kwa carolanne.nehme@scottishrefugeecouncil.org.uk
Simu: 0141 223 7971 **Simu ya rununu:** 07734 030761